

## 12-Swiffaatul-Huruwf - Sifa Za Herufi

### صِفَاتُ الْحُرُوفِ Swiffatul-Huruwf - Sifa za herufi

Maana ya Swiffah: ni namna ambayo hutamkwa herufi, na kwa hali hiyo huweza kutofautisha baina ya herufi zenye kushirikiana katika makhraj na nyengine wakati wa kuzitamka.

Msomaji ataweza kufikia kuisoma Qur-aan kama inavyotakiwa kusomwa kwa kuipa kila herufi haki yake na hilo hatoweza kulifikia mpaka aweze kufikia kuelewa swiffah na makhraj ya kila herufi.

#### Faida ya kuelewa swiffah za herufi:

- Kuweza kuipa kila herufi haki yake katika kutamkwa.
- Kupambanua baina ya herufi ambazo makhraj ni moja mfano: ط ت د au ص na س . Herufi inapotoka katika makhraj yake sawa sawa na ikapewa swiffah yake, ndipo matamshi yanapotoka sawa sawa ipasavyo.
- Kutofautisha baina ya herufi za nguvu na zilizo dhaifu.

#### Swiffah zinagawika katika aina mbili:

صِفَاتُ ذَوَاتِ الْأَضْدَادِ Swiffaatul-dhawaatil-adhwadaad - Swiffah zilizo na kinyume chake

صِفَاتُ الَّتِي لَا ضِدَّ لَهَا Swiffaatul-llatiy laa dhawidda lahaa - Swiffah zisizo na kinyume لها